

Ripoti ya UNEP ya EGR ya mwaka wa 2024

Ujumbe mkuu

Maelezo ya jumla

Kadiri uzalishaji wa gesi ya ukaa unavyofikia viwango vipya vya juu na athari za tabianchi zikizidi kuwa mbaya zaidi duniani, mataifa natayarisha Michango Inayoamuliwa na Taifa NDCs) iliyosasishwa ili kuwasilishwa mapema ya mwaka wa 2025 kabla ya COP30 nchini Brazili. *Ripoti ya Uzalishaji wa Gesi Chafu ya Mwaka wa 2024: Tusiendelee kuongeza joto angani...tafadhali!* imegundua kwamba ili kuepuka mwelekeo wa sasa wa ongezeko la joto zaidi ya nyuzijoto 2 katika kipindi cha karne hii, mataifa ni sharti yatumie COP29 mjini Baku, Azerbaijan, kama njia ya kuongeza ahadi na kuhakikisha NDC mpya kwa pamoja zinaahidi kupunguza karibu nusu ya uzalishaji wa gesi ya ukaa kufikia mwaka wa 2030. Ni sharti yafuatiye na utekelezaji wa haraka wa ahadi, kwa kuzingatia hatua zilizochukuliwa kufikia sasa. Yasipofanya hivyo, lengo la Mkataba wa Paris la kufikia nyuzijoto 1.5 litatoweka ndani ya miaka michache na lengo la kufikia nyuzijoto 2 litakuwa hatarini.

Bado inawezekana kiufundi kuweza kufikia nyuzijoto 1.5, huku nishati ya jua, upepo na misitu ikituma matumaini ya kweli ya kupunguza kwa uzalishaji na utoaji wa hewa chafu haraka. Ili kutimiza uwezo huu, NDC thabiti za kutosha zitahitaji kuungwa mkono haraka na mbinu nzima inayozingatwa na serikali, hatua zinazongeza manufaa ya kijamii na kiuchumi na kimazingira kwa pamoja, ushirikiano ulioimarishwa wa kimataifa unaojumuisha mageuzi ya mfumo wa ufadhili duniani, hatua thabiti za sekta binafsi na angalau uongezekaji mara sita wa ufadhili wa kukabiliana na hali. Mataifa ya G20, haswa wanachama wanaozalisha hewa chafu zaidi, yanahitaji kufanya kazi nzito.

Michango Inayoamuliwa na Taifa (NDCs) iliyosasishwa kwa Mkataba wa Paris, ambayo inatarajiwa kuwasilishwa mapema mwaka ujao kabla ya COP30 nchini Brazili, ni sharti kwa pamoja iahidi na kutekeleza upunguzaji ambao haujawahi kushuhudiwa wa uzalishaji wa gesi ya ukaa kufikia mwaka wa 2030 ili kudumisha lengo la nyuzijoto 1.5.

- Ili kuwa na njia nafuu ya kudhibiti ongezeko la joto duniani lisizidi nyuzijoto 1.5, uzalishaji wa hewa chafu ni sharti upungue kwa asilimia 42 kufikia mwaka wa 2030, ikilinganishwa na viwango vya mwaka wa 2019. Ili kufikia nyuzijoto 2, uzalishaji wa hewa chafu ni sharti upungue kwa asilimia 28 kufikia mwaka wa 2030.
- Kwa kuzingatia mwaka wa 2035 - hatua kuu zinayofuata baada ya mwaka wa 2030 zijumuishwa katika malengo ya NDC - uzalishaji wa hewa chafu ni sharti upungue kwa asilimia 57 kufikia nyuzijoto 1.5 na asilimia 37 kufikia nyuzijoto 2.

- Kwa kuwa uzalishaji wa gesi ya ukaa uliongezeka kwa asilimia 1.3 mwaka baada ya mwaka hadi kiwango cha gigatoni 57.1 za kaboni dioksidi katika mwaka wa 2023, kazi imekuwa ngumu zaidi; asilimia 7.5 ya uzalishaji wa hewa chafu unapaswa kupunguzwa kila mwaka hadi mwaka wa 2035 ili kufikia nyuzijoto 1.5 na asilimia 4 ili kufikia nyuzijoto 2.
- Kila sehemu ya nyuzijoto inayoepukika ni muhimu kwa kuzingatia maisha yanayookolewa, uchumi unaolindwa, uharibifu unaoepukika, bayoanuai inayohifadhiwa na uwezo wa kupunguza kwa haraka kiwango chochote cha joto kinachoongezeka.

Ikiwa NDC za sasa pekee ndizo zitakazotekelezwa na hakuna kujitolea zaidi kutakojumuishwa katika ahadi, hali bora tunayoweza kutarajia kufikia ni janga la ongezeko la joto duniani la hadi nyuzijoto 2.6 katika kipindi cha karne hii.

- Utekelezaji kamili wa NDC zisizo na masharti na zile zilizo na masharti – zilizo na masharti zinahitaji usaidizi kutoka nje – zinaweza kupunguza tu uzalishaji wa hewa chafu unaotarajiwa mwaka wa 2030 kwa asilimia 10, na hivyo kusababisha ubashiri wa hadi nyuzijoto 2.6 za ongezeko la joto.
- Utekelezaji wa NDC za sasa zilizo na masharti utapelekea hadi nyuzijoto 2.8 ya ongezeko la joto.
- Utekelezaji wa sera za sasa pekee utapelekea hadi nyuzijoto 3.1 ya ongezeko la joto.
- Matukio haya yote yanaweza kusababisha athari mbaya zaidi kwa watu, sayari na uchumi, na kupelekea kuhitaji katika siku zijazo uondoaji wa kaboni dioksidi anganikwa gharama za juu na kwa kiwango kikubwa ili kupunguza ongezeko linalotoa shinikizo kwa malengo ya Paris.

Licha ya ukubwa wa kazi iliopo, bado inawezekana kiufundi kupunguza uzalishaji wa hewa chafu kwa kuzingatia lengo la kufia nyuzijoto 1.5.

- Ripoti inaonyesha kuwa pengo la uzalishaji wa hewa chafu kwa mwaka wa 2030 na mwaka wa 2035 linaweza kupunguzwa kwa gharama ya chini ya Dola za Marekani 200 kwa kiwango cha tani ya CO₂.
- Uwezo wa kupunguzwa katika mwaka wa 2030 ni kiwango cha gigatoni 31 za CO₂ – ambacho ni karibu asilimia 52 ya uzalishaji wa gesi ya ukaa duniani katika mwaka wa 2023 – na gigatoni 41 katika mwaka 2035.
- Kuongezeka kwa matumizi ya teknolojia ya nishati ya jua na nishati ya upepo kunaweza pelekea asilimia 27 ya jumla ya uwezo huu wa kupunguza uzalishaji wa hewa chafu katika mwaka wa 2030 na asilimia 38 katika mwaka wa 2035.
- Kushushughilikia misitu kunaweza kupelekea angalau asilimia 20 ya uwezo huu katika miaka hii yote.
- Mambo mengine thabiti ni pamoja na hatua mwafaka, uwekaji umeme na ubadilishaji wa nishati katika sekta za ujenzi, uchukuzi na viwanda.

Kufikia uwezo wa kukabiliana na hali kunahitaji uhamasishaji wa kimataifa wa haraka kwa kiwango na kasi ambayo hushuhudiwa tu baada ya mzozo wa kimataifa.

- Ripoti hii inatoa wito wa kuwa na mfumo unaozingatiwa na serikali nzima, unaozingatia hatua zinazoongeza manufaa ya kijamii na kiuchumi na kimazingira pamoja na kupunguza mwafaka.
- Muhimu pia ni ongezeko la angalau mara sita la uwekezaji wa kukabiliana na hali– unaoungwa mkono na mfumo wa ufadhili duniani na hatua thabiti za sekta binafsi.
- Sio ufadhili wote wa ziada utaongezwa, kwa kuwa uwekezaji unahitajika hata hivyo ili kukidhi mahitaji yanayoongezeka ya nishati na mahitaji mengine ya maendeleo.
- Makadirio ya ongezeko la uwekezaji wa kutozalisha hewa chafu ni dola za Marekani kati ya trilioni 0.9 na trilioni 2.1 kwa mwaka kuanzia mwaka wa 2021 hadi mwaka wa 2050. Kwa muktadha, uchumi duniani na masoko ya fedha yana thamani ya Dola za Marekani trilioni 110 kwa mwaka.

Hatua na uongozi wa G20, haswa na mataifa makubwa zaidi kiuchumi na wazalishaji wakuu wa hewa chafu, zitakuwa muhimu.

- Nchi wanachama wa G20, ukiondoa Umoja wa Afrika, zilichangia asilimia 77 ya uzalishaji wa hewa chafu katika mwaka wa 2023.
- Kuongezwa kwa Umoja wa Afrika kwa G20, hali ambayo inaongeza nchi zaidi ya maradufu kutoka nchi 44 hadi nchi 99, inaleta jumla ya uzalishaji wa hewa chafu hadi asilimia 82 tu - na kuangazia umuhimu wa kutofautisha majukumu kati ya mataifa.
- Kwa vile wanachama wa G20 bado hawako karibu kufikia NDC za sasa, nchi wanachama wanaozalisha hewa chafu nyingi zaidi zinahitaji kuimarisha hatua na kujitolea sasa na katika ahadi mpya.
- Usaidizi thabiti wa kimataifa na ufadhili wa kushughulikia tabianchi ulioimarishwa utakuwa muhimu ili kuhakikisha malengo ya kukabiliana na hali na ya maendeleo yanaweza kutimizwa kwa haki kwa nchi zote wanachama wa G20 na katika ngazi ya kimataifa.

NDC zilizosasisywa ni sharti ziwe zimeundwa vyema, ziwe mahususi na wazi ili kufikia malengo yoyote mapya yaliyowekwa.

- NDC ni sharti zijumuishe gesi zote zilizoordheshwa katika Itifaki ya Kyoto, zijumuishe sekta zote, ziweke malengo mahususi kuhusiana na mwaka wa msingi, na ziwe wazi kuhusu vipengele vilivyo na masharti na visivyo na masharti.
- Ni sharti zieleze jinsi mipango ya kitaifa inavyotoa kipaumbele kwa maendeleo na hatua za kufikia Malengo ya Maendeleo Endelevu inaendana na juhudi kabambe za kupunguza uzalishaji wa hewa chafu.
- Ni sharti zieleze wazi kwa njia inayoeleweka kuhusu jinsi wasilisho linavyoakisi sehemu kubwa ya juhudi na matarajio ya juu zaidi.
- Ni sharti wajumuishe mipango ya kina ya utekelezaji inaozingatia maamuzi ya kuimarisha juhudi za kukabiliana na hali sasa na kwa mwaka wa 2035. Mipango hii inapaswa kujumuisha vigezo vya kissekta, maamuzi mwafaka na uwezekano wa kukabiliana na hali, na mifumo ya tathmini na uwajibikaji.

- Kwa soko linaloibuka na chumi zinazoendelea, NDC zinapaswa kujumuisha maelezo kuhusu njia za utekelezaji wanazohitaji, ikijumuisha mabadiliko ya kitaasisi na sera, na usaidizi wa kimataifa na fedha zinazohitajika.